



Uchanganuzi wa Ubanaji wa Maana za Maneno Katika Jukwaa la "Facebook"

Simon Peter Katui

Chuo Kikuu cha Nairobi, Kenya

Uwasilishaji wa Makala

Kupokelewa: 2025-07-19

Kurekebisha: 2026-01-20

Kukubaliwa: 2026-02-18

Kuchapishwa: 2026-02-24

Maneno Muhimu

Facebook

Maana

Pragmatiki

Ubanaji

Jinsi ya Kurejelea Makala:

Katui, S. P. (2026). Uchanganuzi wa Ubanaji wa Maana za Maneno Katika Jukwaa la "Facebook". *Journal of Kiswahili and Other African Languages*, 4(1), 13-23.

Copyright © 2026



Ikisiri

Makala hii inachanganua ubanaji wa maana za maneno katika jukwaa la *Facebook*. Suala la ubanaji wa maana za maneno katika mawasiliano limewavutia wasomi kadhaa. Hata hivyo, hakuna utafiti ambao umefanyika kuhusu ubanaji wa maana za maneno katika jukwaa la *Facebook*. Makala hii imejikita katika kuchanganua ubanaji wa maana za maneno pamoja na kiini cha matumizi ya ubanaji huo katika jukwaa la *Facebook*. Makala hii iliongozwa na Nadharia ya Semantiki Leksika ya Blutner (1998). Mkabala wa makala hii ni wa kimaelezo. Sampuli ya utafiti huu ilikuwa ya kimakusudi, ambapo tuliteua vikundi vitatu vya mawasiliano katika jukwaa la *Facebook* kwa hiari. Data iliyotumika katika makala hii ilikusanywa kati ya mwezi Aprili na Oktoba mwaka wa 2020. Vikundi vya mawasiliano kwenye jukwaa la *Facebook* vilitumika. Data hii ilikusanywa kwa ajili ya tasnifu ya uzamili iliyoshughulikia suala la Uchanganuzi wa Kipragmatiki wa Maana ya Mawasiliano katika Jukwaa la *Facebook*. Tulipitia kurasa za makundi ya mawasiliano katika jukwaa la *Facebook* na kunakili data husika. Tulichanganua data tuliyoinakili ili kupata lengo la ubanaji wa maana za maneno kwenye jukwaa la *Facebook*. Data iliyokusanywa kuhusu mada hii inaonesha kwamba mawasiliano katika jukwaa la *Facebook* husheheni matumizi ya ubanaji wa maana za maneno. Kwa kuzingatia Mkabala wa Pragmatiki, makala hii inaonesha kwamba watu hutumia ubanaji wa maana za maneno. Watu hubana maana za maneno kwa ajili ya kusetiri ujumbe na kuhifadhi heshima na taadhima kwa wanakikundi. Maana za maneno hubanwa kulingana na mazingira ya usemi husika kwa nia ya kuleta umoja.

Utangulizi

Binadamu hufanya mawasiliano kupitia njia kadha wa kadha ambapo kuna mawasiliano kupitia njia ya mdomo, radio, na televisheni. Pia, kuna mawasiliano ambayo yanafanyika kupitia majukwaa ya kidigitali kama vile *Twita*, *Whatsapp*, na *Facebook* na kadhalika. Makala hii inashughulikia ubanaji wa maana za maneno na kiini chake kwenye mawasiliano ya jukwaa la *Facebook*. Kulingana na Blutner (2000), ubanaji ni hali ya mzungumzaji kutumia faridi za kileksika kupitisha maana, ambayo imebanwa kuliko ile maana, ambayo imesimbwa kisemantiki. Kwa mfano, kisemantiki, Kiswahili ni lugha mojawapo kati ya lugha nyinginezo ulimwenguni na, pia, Kiswahili ni neno ambalo lina maana ya somo mojawapo katika mtaala wa elimu ulimwenguni. *Facebook* ni jukwaa linalotumiwa kimawasiliano ambapo inatumika na wawasilianaji kote ulimwenguni kwa sababu za kuafikia mahitaji ya kimaisha.



Jukwaa la *Facebook* limeweza kuwavutia wasomi kama vile Kiunga (2016), Katui (2020), Annah (2023) na Nkumbo na wenzake (2019), ambao wamezamia katika masuala mbalimbali ya kiusomi kama vile; sifa za lugha tumizi katika *Facebook*, athari zake, maana ya mawasiliano, maudhui katika matangazo ya ngono salama, na upanuzi wa maana. Hata hivyo, suala la ubanaji wa maana za maneno katika muktadha wa *Facebook* halijajitokeza kwenye mawasiliano. Hivyo, makala hii inajadili ubanaji wa maana za maneno katika mawasiliano ya jukwaa la *Facebook*. Tumechunguza suala la ubanaji wa maana kimawasiliano kwa kuongozwa na misingi ya Nadharia ya Blutner (1998). Nadharia hii inajikita katika uchanganuzi wa mageuzi ya maana katika muktadha wa mawasiliano; yaani maana za maneno kusimbwa, kubanika, kupanuliwa, na kukisiwa. Tumeweza kuegemeza nadharia hii kwenye miktadha ya mazungumzo ili kupata picha jumishi ya ubanaji wa maana za maneno kwenye mawasiliano katika jukwaa la *Facebook*.

Horn na Ward (2004), wanadai kuwa, ubanaji ni mchakato wa kiwango kikubwa, kwani ni mchakato ambao unaweza kusawazishwa kutegemea muktadha wa matumizi ya lugha. Maelezo haya yanafanana na mawazo ya Blutner katika nadharia yake ya Pragmatiki Leksika (1998) iliyotungoza katika makala hii. Mawazo yana umuhimu mkubwa katika utafiti huu.

Mkude (1995), anachanganua maneno ambayo yana maana sawa kwa kuisitiza haja ya kuangalia muktadha. Anaeleza kwamba kimuktadha, unaweza kuunganisha maneno au vipashio vya sentensi ili kupata maana. Anafafanua kwa kutoa mfano mzuri na anatumia sentensi inayosema: "Aliingia kwa tabasamu iliyong'aa wajihini" Dhana ya neno iliyong'aa wajihini ni kama ifuatavyo: Iliyometameta usoni, iliyoangaza usoni, iliyomulika usoni, iliyowaka usoni, iliyovutia usoni au iliyowaa usoni. Hivyo basi, bila muktadha ni vigumu kubaini visawe vya neno ng'aa jinsi lilivyotumika katika mawasiliano. Maelezo haya ni muhimu katika utafiti huu kwa kuwa yatatuwezesha kupata uelewa wa ubanaji wa maana katika mawasiliano.

Ochoki (2010), alichunguza usimbwaji wa fahiwa katika nyimbo za *Hip hop* zinazoimbwa nchini Kenya. Alitumia mchakato wa upanuzi na ubanaji wa maana katika kufafanua usimbwaji wa kimaana. Utafiti huo ni muhimu katika makala hii kwa sababu ulituwezesha kupata mwongozo kuhusu maana za maneno yanayobanwa kwenye mawasiliano. Kiunga (2016), alitafiti kuhusu maana ya usemi na mazungumzo katika mitandao ya kijamii, hususan *Facebook* na *Twitter*. Katika utafiti wake aliweza kubainisha kuwa lugha katika mitandao ya kijamii ina sifa na majukumu yake maalum. Isitoshe, mitandao ya kijamii ina nafasi kubwa katika jamii kwa sababu inawaunganisha watu wa matabaka mbalimbali. Mawazo haya ni ya muhimu kwa sababu yalituwezesha kuelewa matumizi ya lugha kwenye jukwaa la *Facebook*.

Naye Asiko (2019), alitafiti kuhusu ushawishi wa kiasi cha habari kinachopitishwa katika tafsiri. Alibainisha kwamba ubanaji husababisha upotoshi wa maana kwani huonesha uwezo alionao mtu katika matumizi ya lugha. Mawazo haya yalitufaa katika makala hii kwa sababu yalituwezesha kupata uelewa wa ubanaji wa maana za maneno kwenye mawasiliano. Kwa upande mwingine, Kirui (2021), katika utafiti wake wa urejelezi katika gazeti la *Taifa Leo* mtazamo wa Pragmatiki, alibainisha kuwa ubanaji wa maana ya lugha hutumika katika mchakato wa kufasiri maana katika mawasiliano kwenye gazeti. Utafiti huu ulikuwa na manufaa katika makala hii kwa sababu ulitupa uelewa wa kutambua maneno yaliyobanwa kimaana kwenye mazungumzo ya jukwaa la *Facebook*.

Katika utafiti wake, Annah (2023), anasema kwamba, kuna tofauti baina ya lugha ya kandanda inayotumiwa nchini Kenya na Tanzania kwa misingi ya uchanganuzi ndimi, uhawilishaji wa msimbo, matamshi ya maneno na msamiati unaotumika. Hata hivyo, inapokuja katika misingi ya lugha hatupati tofauti kubwa baina ya lugha ya kandanda ya Kenya na Tanzania. Pia, upanuzi na ubanaji wa maana za maneno hujitokeza kote Kenya na Tanzania kwa sababu za kiisimu. Utafiti



huo ulikuwa na manufaa makubwa katika makala hii kwa sababu, ulituwezesha kufahamu kiini cha ubanaji wa maana za maneno katika jukwaa la *Facebook*.

Msingi wa Kinadharia

Makala hii imeongozwa na Nadharia ya Pragmatiki Leksika iliyoasisiwa na Blutner (1998) na kuendelezwa na Wilson (2003). Pia, nadharia hii iliendelezwa zaidi na Wilson na Carson (2007). Kimsingi, nadharia hii inazungumzia mpangilio na ufafanuzi wa fenomena za kipragmatiki ambazo zinaambatanishwa na semantiki chini ya vipashio vya kileksika. Blutner (keshatajwa) anatoa mtazamo wake kuhusu lugha kuwa; vipashio vya lugha vinachanganuliwa kwa njia maalum kulingana na muktadha wa matumizi ya lugha. Nadharia hii inajikita katika uchanganuzi wa mageuzi ya maana katika muktadha, yaani maana za maneno kusimbwa, kubanika, kupanuliwa na kukisiwa. Pragmatiki Leksika inatoa maelezo kwamba, faridi za kileksika za lugha zinachanganuliwa kiutaratibu na kufasiriwa kulingana na muktadha mahususi wa mawasiliano. Mchango wa Semantiki katika ufasiri wa maana ya jumla ya neno unabanwa kuliko ilivyodhaniwa awali kwani pragmatiki leksika inafafanua na kuelezea fenomena za kipragmatiki ambazo zimeshikamana na semantiki chini ya elementi za kileksika.

Mihimili ya Nadharia ya Pragmatiki Leksika

Semantiki Leksika

Semantiki leksika inashughulika na dhana ya neno hususan dhana ya msingi. Maneno huchukuliwa kwa ajili ya kuonesha kitu fulani kwa kuzingatia mtazamo mahususi wa semantiki leksika. Utetezi wa Mmbawanga (2010), ni kwamba, vitengo vya dhana katika semantiki leksika ni vitengo vya kileksika ambavyo kwavyo mzungumzaji huweza kuongezea kwa mfululizo katika maisha pamoja na ujifunzaji wa dhana ya maneno mapya na dhana yake. Mhimili huu ulikuwa wa msaada mkuu katika makala hii kwa kuwa ulituwezesha kupata maana ya msingi ya neno, ndipo tuweze kuangazia maana iliyosimbwa kisemantiki, yaani, maana iliyobanwa, maana iliyopanuliwa, na maana inayoweza kukadiriwa kulingana na muktadha wa mazungumzo.

Michakato ya Pragmatiki leksika

Ubanaji wa kileksika

Ubanaji wa kileksika ni mchakato ambao unajihusisha na matumizi ya neno au kirai katika kuonesha dhana mahususi zaidi ya maana iliyosimbwa kiisimu. Utafiti huu unakubaliana na ufafanuzi huu na kushadidia kuwa maana pana ya neno ndiyo iliyosimbwa kiisimu kwani wakati ubanaji wa maneno kimuundo na kimaana unafanywa, tunapata dhana ndogo katika muktadha wa mazungumzo.

Horn na Ward (2004), wanadai kuwa, ubanaji ni wa kiwango kikubwa kwani, ni mchakato unaoweza kusawazishwa na hutegemea muktadha unaohusika. Maana iliyosimbwa inaweza kubanwa katika dhana tofauti kutegemea muktadha wa kimawasiliano. Kwa mfano, Katui ana Kiswahili. Neno Kiswahili lina maana pana kwani, linaweza kumaanisha kuwa mtu huyu ni mzungumzaji mwema wa lugha ya Kiswahili, ni mjanja au ana ufasaha katika somo la Kiswahili. Pia, ni mjuzi wa masuala fulani. Kwa hiyo, ni lazima maana iliyosimbwa katika mawasiliano iweze kufasiriwa kimuktadha.



Upanuzi wa Kileksika

Upanuzi wa kileksika ni mchakato ambao kwao dhana ya neno hupanuka kwani, neno linamaanisha kila kitu kilichokuwa kikimaanishwa na kuweza kuongeza fahiwa nyingine kwa hiyo, fahiwa ya neno hupanuka.

Kisio la maana

Haya ni mabadiliko ya maana ambayo kwayo leksimu zilizo thabiti kwa namna fulani hupanuliwa mwishoni na kujumuisha mawanda ya makundi ambayo kwa yakini yanapatikana nje ya maana yake kamilifu kiisimu. Michakato hii ilitufaa katika kuandika makala hii kwa kuwa ilitupa mwafaka bayana kuhusu ubanaji wa maana kipragmatiki.

Mbinu za Utafiti

Utafiti huu ulitumia mkabala wa kimaalezo. Hii ni njia ya kukusanya data na kuichambua kwa njia ya maelezo ambapo takwimu huwa hazitumiki. Data ambazo zimetumika katika makala hii zilikusanywa katika makundi teule ya jukwaa la *Facebook*. Tuliweza kusoma na kupakua data kutoka kurasa za *Facebook*.

Tulitumia ujumbe wa watu ambao huwasiliana kupitia majukwaa ya makundi yafuatayo kama sampuli lengwa: *Kundi la Kenyatta University Students, Kenya University Organization na Kenyatta University Comrades*. Sampuli ilichaguliwa kimakusudi ili kupata data iliosaidia kufikia lengo la makala hii. Tuliychagua makundi matatu kwa sababu ya upanuzi wa mawanda ya utafiti. Uchanganuzi wetu wa ubanaji wa maana ya maneno ya mawasiliano katika jukwaa la *Facebook* ulikuwa wa kielezi kwa matumizi ya Nadharia ya Pragmatiki Leksika ya Blutner (1998). Data zilipangwa katika kategoria za ubanaji wa maana za maneno kimuktadha na kuwasilishwa kimaalezo. Matokeo yalionesha kwamba wanafunzi huwasiliana kwa matumizi ya ubanaji wa maana za maneno katika jukwaa la *Facebook* kwa sababu za kuusetiri ujumbe na kuhifadhi heshima na taadhima kwa wanakikundi husika.

Ubanaji wa Maana katika Mawasiliano ya Jukwaa la Facebook

Ubanaji wa maana za maneno kileksika ni kutumia faridi leksika kwa ajili ya kupitisha dhana ambayo imebanwa zaidi kuliko ilivyowasilishwa. Maana hii finyu ni lazima iwe na uhusiano na mandhari ambayo yanahusika kwa sababu, maana iliyosimbwa inaweza kubanwa katika maana tofauti kutegemea muktadha wa matumizi.

Katika mchakato huu neno linatumiwa kuonesha dhana mahususi zaidi kuliko dhana iliyosimbwa kisemantiki na hivyo kusababisha kutokea kwa ufinyu wa maana halisi ya kiisimu.



Naomi Mwendu

K.U. Comrades Forum

18 Machi saa 08:08 ·

Taking somebody from the village is easy but kuitoa village yenyewe kutoka kwa mtu ni noma, kwa sababu watu wengi huwazia masuala waliyoelemishwa na Somo wao halafu inakuwa ni Mlima kuachana na mwiko, hata hivyo. Kutema some of the village issues inakuwa suala ninalohitaji kutadisi kwa siku nyingi. Uvillage unawafanya wanagenzi wengi kuinamisha Sheria za shule ba kufanya mambo tumbi yasiyohesabika aushini mwa waja. Wilson (2003) anadai kuwa ubanaji wa kileksika ni mchakato unaohusu matumizi ya neno katika kuonesha maana mahususi kuliko maana iliyosimbwa kiisimu.

Makala hii inashadidia mawazo haya kuwa maana pana ya neno, ndiyo iliyosimbwa kwa kuwa wakati ubanaji wa maana za maneno unafanyika tunapata dhana ndogo katika muktadha wa



mazungumzo. Katika mazungumzo haya, kuna matumizi ya neno 'somo'. Kwa mujibu wa TUKI (1990), neno hili hutumika kuamaanisha maarifa ambayo hupangiliwa katika muktadha maalumu au mtu anapojifunza darasani au vyuoni, au mambo mazuri ama mabaya anayoyapata mtu kwa kuangalia au kupatwa na jambo lililomkabili. Somo, pia, ni rafiki wa karibu, mwandani au shoga, mtu ambaye jina lake linalandana na lako. Neno hili pia, linatumiwa kumaanisha mtu anayewapa mafunzo maalumu ya jando na unyago vijana waliobalehe. Tukitazama muktadha wa mawasiliano haya, tunaona kuwa, mwanafunzi huyu ameibana maana ya jumbe hizi kwa maana ya mtu ambaye huwapatia vijana mafunzo maalumu ya jando na unyago, walio komaa. Hivyo basi maana ya neno hili imebanwa na kutupa maana zingine kimakusudi. Ubanaji huu unafanyika kwa lengo la kuusetiri ujumbe kwa wanakikundi na kuhifadhi heshima na taadhima kwa wanakikundi husika.

Isitoshe, katika mawasiliano haya, kuna matumizi ya neno 'Mwiko'. Kwa mujibu wa TUKI (1990), neno hili linamaanisha kifa ambacho hutoka katika mti na hutumika kusonga ugali, kibati chenye mpini kitumiwacho na mjenzi kuchotea udongo na sementi kupigia plasta na kulainisha kuta wakati wa kuujenga. Pia, mwiko ni kitu au jambo au hata neno ambalo mtu anakatazwa kulifanya, kulisema ama kula kwa sababu ya kuogopa kudhurika kiafya au kufedheheka katika jamii ama jambo ambalo mtu hawezi kulifanya kutokana na imani, msimamo wake au mazoea tu. Makala hii inashadidia mawazo ya Blutner (1998) kuwa, ubanaji wa maana za maneno kileksika ni kutumia faridi leksika kwa ajili ya kupitisha dhana ambayo imebanwa zaidi kuliko ilivyowasilishwa. Katika muktadha wa mawasiliano haya ya Mwendu, maana inayolengwa ni kitu au jambo au hata neno ambalo mtu anakatazwa kulifanya, kulisema, ama kula kwa sababu ya kuogopa kudhurika kiafya au kufedheheka katika jamii, au jambo ambalo mtu hawezi kulifanya kutokana na imani yake. Hivyo basi, maana ya neno hili imebanwa na kutupa maana zingine za nje. Wanafunzi hawa huweza kutumia mchakato huu wa ubanaji wa kimaana kwa makusudi kwa lengo la kuusetiri ujumbe na kuhifadhi heshima na taadhima kwa wanakikundi husika.



Naomi Mwendu

K.U. Comrades Forum

Jana saa 02:30 ·

Elimu ni nyenzo muhimu sana maishani mwa mja. Lakini Mburukenge wengine walionyesha suala hili kisogo pasi kujua kuwa watakuja teseka mwamboni. Jua linapochomoza inafaa kila MTU awajibike ipasavyo. La mno ni kuwa, kwa nini? Watesi huamua kuwa Mburukenge.

Wilson (2003) anadai kuwa, ubanaji wa kileksika ni mchakato unaohusu matumizi ya neno katika kuonesha dhana mahususi kuliko maana iliyosimbwa ya kiisimu. Makala hii inakubaliana na maelezo haya na kushadidia kwamba maana pana ndiyo iliyosimbwa kiisimu kwa sababu ubanaji wa maneno kimuundo na kimaana unapofanywa tunapata dhana ndogo katika muktadha wa mazungumzo.

Katika mawasiliano ya Naomi kwenye jukwaa la Facebook, kuna matumizi ya neno 'jua'. Neno hilo limetumika kwa maana ya kuwa na ufahamu katika sentensi 'pasi kujua kuwa watakuja kuteseka siku za usoni.' Hivyo basi, maana ya neno hili inabanwa na kuiacha maana nyingine nje. Isitoshe katika muktadha huu, mwanafunzi huyu anaendelea kuleta maana ya pili ya neno 'jua' kama nyota kubwa kuliko zote, yenye uwezo wa kutoa mwanga na kusababisha joto duniani, ambayo hutokea wakati wa asubuhi na kuzama wakati wa jioni. Haya yanadhihirika katika kijejezi 'Jua linapochomoza inafaa kila MTU awajibike.' Hivyo basi, maana ya neno hili inabanwa na kuacha

maana nyingine nje. Hapa mwasilianaji huyu ametumia mkakati huu kwa sababu za kuusetiri ujumbe na kuhifadhi heshima na taadhima kwa wanakikundi husika.



Boniface Lens Ochieng

Kenyan University Students (UON, SEKU, MU, MMUST, KU, JKUAT and Egerton)

9 Machi saa 21:54 ·

Maudhui haya hayapatikani kwa sasa

Hili linapofanyika, kwa kawaida ni kwa sababu miliki aliishiriki tu kwa kikundi kidogo cha watu, kubadilisha anayeweza kuiona au limefutwa.

Katika chapisho hili, Boniface Lens Ochieng anawasiliana kwa matumizi ya neno ‘**miliki**’. Kisemantiki, neno hili lina fahiwa nyingi kama vile: miliki ni mali aliyo nayo mtu au shirika, nchi ambayo mtawala ana mamlaka nayo, aghalabu huongozwa na malkia au mfalme na pia miliki ni kuwa na mali au kitu kinachothaminiwa. Blutner (1998), anatoa mtazamo wake kuhusu Ubanaji wa maana za maneno kuwa vipashio vya lugha vinachanganuliwa kwa njia maalum kulingana na muktadha.

Makala hii nashadidia mtazamo huo kwa sababu, katika muktadha huu wa kimawasiliano, Boniface anatumia neno hili kuleta maana ya kuwa na kitu kinachothaminiwa. Hivyo basi, neno hili limebanwa kimaana na kutupa nje maana nyinginezo za neno hili.

Hata hivyo, matumizi ya neno ni kwa sababu za kuusetiri ujumbe na kuhifadhi heshima na taadhima kwa wanakikundi husika.



Cleophas Nyongesa

Kenyan University Students (UON, SEKU, MU, MMUST, KU, JKUAT and Egerton)

Asante kunipa nafasi kuwa sehemu yenu ili tutambe kwenye nyanja za taaluma pamoja.

Katika mawasiliano ya Cleophas, kuna matumizi ya neno ‘**tamba**’. Kulingana na Blutner (1998) ubanaji ni hali ya mzungumzaji kutumia faridi za kileksika kupitisha maana iliyobanwa kuliko maana iliyosimbwa kimantiki. Makala hii inashadidia mawazo haya kwani, kisemantiki, neno hili lina fahiwa nyingi kama vile: Zunguka huku na kule ukijisifu na kujigamba, na elezea au simulia hadithi kwa watu wengine. Pia, neno hili hutumika kumaanisha hali ya kukosa mpinzani kwenye mashindano au kazi fulani. Katika muktadha wa mawasiliano haya, mwanafunzi huyu anatumia usemi huu: ‘Asante kwa kunipa nafasi kuwa sehemu yenu ili tutambe kwenye nyanja za taaluma pamoja’ Tunapojikita kwenye muktadha huu wa mawasiliano, tanabaini kwamba neno hili limetumika kwa maana ya kuelezea au kusimulia hadithi kwa watu wengine au kutongoa. Kwa hiyo, neno hili limebanwa kwa maana hii na kutupatia maana nyingine ya nje. Ubanaji huu ni wa makusudi ukiwa na lengo la kuusetiri ujumbe na kuhifadhi heshima na taadhima kwa wanakikundi husika.



Cleophas Nyongesa

Kenyan University Students (UON, SEKU, MU, MMUST, KU, JKUAT and Egerton)

Ilikuwa ni mguu niponye, kuchupa, kufokeana na vyombo vya dola kuonyesha ubabe wao katika maeneo yaliyokuwa na chaguzi ndogo. Baadhi ya waheshimwa walijipata wametwa nguvuni kwa kucheza ngoma mbaya siku ya kutambua mbivu na mbichi.

Katika mawasiliano haya, mwanafunzi huyu anawasiliana akitumia neno 'kuchupa', ambacho ni kitenzi kilichoundwa kutokana na nomino 'chupa'. Kimsingi, neno hili lina fahiwa zifuatazo: 'Ruka' kutoka sehemu moja hadi nyingine, chombo cha kuwekea vinywaji, na hali ya nguo kuwa fupi. Katika muktadha wa mawasiliano haya, neno hili limetumika kwa maana ya kuruka kutoka sehemu moja hadi nyingine, kwani, mwanafunzi huyu katika mawasiliano yake ameweza kubana neno hilo kwa maana moja (kuruka kutoka sehemu moja hadi nyingine), na kutupa nje maana nyingine za neno chupa. Ubanaji huu unashadidia mawazo ya Blutner (1990) kuwa ubanaji ni hali ya mzungumzaji kutumia faridi za kileksika kupitisha maana inayobanwa kuliko maana iliyosimbwa. Ubanaji huu unafanyika kwa ajili ya kuusetiri ujumbe na kuhifadhi heshima na taadhima kwa wanakikundi.



Kennedy Shavanga

Kenyan University Students (UON, SEKU, MU, MMUST, KU, JKUAT and Egerton)

3 Machi saa 21:28 ·

Wanao mtegemea Bwana Yesu huwa wamejihami kwa neno ambalo huwapigania katika maelfu na maelfu ya vita.

2Faith Nekesa na Christopher Masengeli

Horn.L. (2005) anadai kwamba, ubanaji wa maana za maneno ni wa kiwango kikubwa kwa sababu ni mchakato unaoweza kusawazishwa kwa kutegemea muktadha. Makala hii inakubaliana na mawazo haya, kwani, katika muktadha wa mawasiliano haya, mwanafunzi huyu anatumia neno 'Bwana' katika kuwasilisha ujumbe wake. Neno "Bwana" lina maana kadha kama vile: Mwajiri wa mtu, mume wa mtu, tajiri, na maana nyinginezo. Hata hivyo, katika muktadha wa mawasiliano haya ya Shavanga, neno hili linafasiriwa kwa maana ya Yesu Mwana wa Mungu. Hivyo, katika muktadha huu neno hili linabanwa kimaana japo lina maana nyingine lakini katika muktadha huu maana nyingine zote zimefungiwa nje ili maana moja pekee, ambayo ni Yesu, itiliwe maanani. Lengo la ubanaji huu ni kuusetiri ujumbe na kuhifadhi heshima na taadhima kwa wanakikundi husika.



Steve Juma

Kenyan University Students (UON, SEKU, MU, MMUST, KU, JKUAT and Egerton)

Sala kwa Bwana Yesu iliofanywa na Askofu chuoni mwetu (UoN), iliwafanya watumia unga na wapiga maji kumwona Yesu.

Katika mawasiliano haya, mwanafunzi huyu ameweza kutumia neno 'Bwana' kwa kubana maana kama ilivyoelezwa hapo juu katika mawasiliano ya shavanga. Vilevile, kuna matumizi ya neno



'unga'. Neno hilo lina maana ya kitu kilichosagwa na kuwa vumbivumbi. Katika muktadha wa kawaida, neno 'unga' linajumuisha vitu vingi vya unga kama vile, unga wa mahindi, unga wa wimbi, unga wa mawe, na kadhalika. Hata hivyo, katika muktadha wa mawasiliano haya, neno hili limeweza kubanwa kumaanisha mihadarati kama vile, kokeini dawa ya kulevya ambayo ni ungaunga na, kwa hivyo, maana nyingine zimeweza kuachwa nje. Isitoshe, kuna matumizi ya neno 'maji'. Neno hilo linatumika kwa maana ya vitu viowevu kama vile, sharubati, pombe, maji ya kunywa, na nyinginezo. Katika muktadha wa mawasiliano haya, neno hili limebanwa kwa maana ya pombe na kutupa maana nyingine nje. Makala hii inakubaliana na Blutner (1998) anayedai kuwa wakati mwingine maana za maneno hubanwa kulingana na muktadha wa mazungumzo. Ubanaji huu umeweza kufanyika kwa lengo la kuusetiri ujumbe huu kwa wanakikundi pekee na kuhifadhi heshima na taadhima kwa wanakikundi husika.



Kennedy Shavanga

Kenyan university students (UON, SEKU, MU, MMUST, KU, JKUAT and Egerton)

9 Machi saa 22:23 ·

Mwaa ya gharika ni chumo kwa wakulima wa mahindi pamiwe na miwa, ambacho ni kinaya kwa wakulima wa nyanya. Rasharasha huwafanya wasiopenda kazi kuhema kwa kutafuta mtaji nao wanaopenda vya dezodezo hubaki kikawaida wakijua kwamba wataendelea kuwa kupe kwa mahuluki wenye idili. Ni heri wasomi waoyuo kuwapiga msasa wanagenxi wao ili wasijute maishani na pia wawe dira ya ulimwengu katika siku za mwambo.

Wilson na Carson (2007), wanadai kuwa, Nadharia ya Pragmatiki Leksika inazungumzia mpangilio na ufafanuzi wa fenomena za kipragmatiki ambazo zinaambatanishwa na Semantiki chini ya vipashio vya kileksika. Makala hii inashadidia mawazo haya. Katika mawasiliano haya ya *Facebook*, mwanafunzi huyu anawasiliana kwa matumizi ya neno 'nyanya'. Kimsingi, neno hili hutumika kwa maana mbili, ambazo ni: Mamaye wazazi wangu, na aina ya mboga. Lakini katika muktadha huu wa mawasiliano ya jukwaa la *Facebook*, neno hili limebanwa kwa maana ya aina ya mboga na kutupa maana nyingine ya nje ya neno nyanya. Kusudi la ubanaji huu ni kuusetiri ujumbe na kuhifadhi heshima na taadhima kwa wanakikundi husika. Isitoshe, ubanaji huu ni wa kimaadili.

Vilevile, kuna matumizi ya neno 'dira' ambapo kiisimu neno hili lina fahiwa nyingi kama vile: - Kifaa chenye kuonesha pande za dunia kinachotumiwa na wasafiri, hasa wa anga na baharini kuwawezesha kutambua upande ambao wanaelekea, mawazo anayojiwekea mtu au kikundi cha watu kuhusu namna ya kutekeleza jambo fulani, na nguo ndefu inayofanana na kanzu ivaliwayo na wanawake ambayo haikugawanywa katika eneo kati ya kifua na kiuno. Pia, neno dira linamaanisha hali ya kuondoa nywele kichwani kwa kutumia kifaa kama mkasi au wembe. Katika muktadha wa mawasiliano haya, neno hili limebanwa kwa maana ya mawazo anayojiwekea mtu au kikundi cha watu kuhusu namna ya kutekeleza jambo fulani. Kwa hiyo, maana nyingine imetupwa nje. Ubanaji huu unatumika hapa kwa misingi ya kuhimiza na kuweka wanakikundi pamoja. Isitoshe, ubanaji huu unatumika kwa ajili ya kuusetiri ujumbe huu na kuhifadhi heshima na taadhima kwa wanakikundi.



Vincent Kasembeli

K.U. - Comrades Forum

Saa 1 ·

Hatihati za mamia ya wanasisia kuwatayarisha baadhi ya wanamgambo Na panga pamoja Na rungu ili kuzua rabsha katika uchaguzi zinaitenga dimokrasia katika nchi nyingi. This is not required in a civilised nation jameni...!

Katika mawasiliano ya Kasembeli katika *jukwaa la Facebook*, kuna matumizi ya neno '**panga**'. Kiisimu neno hili lina fahiwa nyingi kama vile: Eneo maalumu ambalo limeteuliwa kwa minajili ya kufanyiwa shughuli za matambiko, kifaa cha kukatia vitu, aghalabu miti na ambacho kinafanana na kisu kikubwa kilicho na makali upande mmoja, na mahali ambapo panaaminiwa kuwa pana mizimu na watu ambapo hupatumia kufanya matambiko, aghalabu pangoni, mtoni, milimani au chini ya mti mkubwa. Pia, neno hilo linamaanisha, kiumbe mdogo wa baharini ambaye ana umbo la bapa na anayependa kujificha kwenye mchanga, kifaa ambacho kinatumika kukinga tope kwenye gari, baiskeli au pikipiki ili mpandaji asichafuke, na shimo katika ardhi lenye maji ambayo hayakauki. Vilevile, neno '**panga**' linamaanisha, ishi katika nyumba au chumba cha mtu kwa makubaliano maalumu ambayo ni ya kumlipa kodi kwa mwezi ama kipindi fulani, weka vitu, ama kitu kwa mpangilio na utaratibu ambao unatakikana, kukubaliana kwa jambo fulani kwa ajili ya kulitekeleza, kaa katika hali ya upweke au ukiwa, na ishi na mwanamke au mwanamme bila kuwa na ndoa. Neno hilo, pia, linamaanisha hali ya kushikilia mtoto vizuri ili aweze kujisaidia. Makala hii imekubaliana na mawazo ya Blutner (1998) anayedai kuwa maana za maneno hubanwa kulingana na muktadha wa mazungumzo. Katika muktadha wa mawasiliano haya, neno hili limebanwa kwa maana ya kifaa cha kukatia vitu aghalabu miti na ambacho kinafanana na kisu kikubwa chenye makali. Ubanaji huu ni wa kulenga wanarika katika kikundi cha kimawasiliano na kuhifadhi heshima na taadhima yao.

Vilevile, katika mawasiliano haya mwanafunzi huyu amewasilisha ujumbe wake kwa matumizi ya neno '**tenga**'. Kisemantiki neno hili hutumika kumaanisha aina ya kapu ambalo linatengenezwa kwa mianzi au minyaa, hali ya kuweka pembeni au kando, bagua mtu, andaa vitu kama chakula na samaki mkubwa jamii ya papa ambaye ana mwiba mkubwa na umbo la bapa ambaye anayeishi baharini. Katika muktadha wa mawasiliano haya, neno hili limebanwa kumaanisha maana ya kuweka pembeni au kando masuala ya kidemokrasia. Ubanaji huu unafanywa kimaksudi kwa lengo la kuusetiri ujumbe wakimawasiliano kwa wanakikundi kusudiwa. Ubanaji huu pia ni wa kuhifadhi heshima na taadhima kwa wanakikundi.



Eddy Gar

Kenya Universities Student Organisation

11 Aprili saa 12:42 ·

Natafuta bibi. Nipewe number pliz

*Katika mawasiliano haya, mwanafunzi huyu anawasiliana kwa matumizi ya neno '**bibi**'. Neno ambalo kimsingi lina fahiwa nyingi kama vile: Mzazi wa kike aliyemzaa baba au mama, yaani nyanya. Pia, ni jina la heshima linalotumiwa kumwita mwanamke.*



Katika muktadha wa mawasiliano haya, neno hili limebanwa kwa maana ya jina la heshima la kumwita mwanamke. Ubanaji huu unafanyika hapa kwa sababu ya kulenga ujumbe kusudiwa kwa wanakikundi.



Aligura E.A.

Kenya Universities Student Organisation



· 11 Aprili saa 21:48 ·

Sai Apa Yunivasithy Bei Ya Nyanya Inacompete Na Unga. Uhuru Fungua 🙄

Katika mawasiliano haya ya *Facebook*, mwanafunzi huyu anawasiliana kwa matumizi ya neno 'nyanya' Kimsingi, katika muktadha wa kawaida, neno hili hutumika kumaanisha mamaye wazazi wangu na aina ya mboga. Lakini katika muktadha huu wa mawasiliano ya jukwaa la *Facebook*, neno hili limebanwa kwa maana ya aina ya mboga na kutupa maana nyingine ya neno nyanya nje. Makala hii inakubaliana na mawazo ya Horn na Ward (2004) ambao wanadai kuwa ubanaji ni wa kiwango kikubwa kwani, ni mchakato ambao unaweza kusawazishwa kwa kutegemea muktadha. Ubanaji huu umetumika hapa kwa lengo la kuusetitiri ujumbe kwa wanakikundi.

Isitoshe, katika mawasiliano haya kuna matumizi ya neno 'unga' ambalo lina maana ya kitu kilichosagwa na kuwa vumbivumbi. Katika muktadha wa kawaida, neno hili linatumika kujumuisha vitu vingi ambavyo vimesagwa kama vile; unga wa mahindi, unga wa wimbi, na kadhalika. Hata hivyo, neno unga limeweza kubanwa katika muktadha wa mawasiliano haya ya jukwaa la *Facebook* kumaanisha mahindi yaliyosagwa na kuwa vumbivumbi, yaani chakula. Ubanaji huu umetumika kwa maana ya kuusetitiri ujumbe huu na kuhifadhi heshima na taadhima kwa wanakikundi.

Hitimisho

Makala hii imebaini kuwa *Facebook* ni jukwaa ambalo linatumika kimawasiliano na watu wa matabaka mbalimbali. *Facebook* hutumika kwa ajili ya kuupitisha ujumbe kimawasiliano na kuafikia haja za kila siku maishani. Katika shughuli ya kutagusana, binadamu hutumia lugha kwa njia ya kipekee ambapo maana za maneno hubanwa kwenye mawasiliano. Hata hivyo maana kusudiwa inabaki kwa wafasiri wa ujumbe na watumiaji lugha kwenye muktadha ya mawasiliano husika.

Tumeweza kupitia kurasa za makundi ya wanafunzi wa vyuo vikuu kwenye jukwaa la *Facebook* na kubaini kwamba, wanafunzi wengi huweza kutumia mikakati ya ubanaji wa maana za maneno kwenye mitagusano yao. Watu hubana maana za maneno katika mazungumzo kwa malengo ya kibinafsi, kwa hiyo ili kupata uelewa wa mazungumzo hayo, nilazima uyafasiri kimuktadha. Hata hivyo makala hii imeshuhudia kwamba ubanaji wa maana za maneno kwenye mawasiliano, una kusudi la kuhifadhi ujumbe kwa wanakikundi na kuleta umoja kwa wawasilianaji. Kwa upande mwingine, watu hutumia ubanaji wa maana za maneno kwa lengo la kuusetitiri ujumbe wa kimawasiliano kwa wanakikundi. Mwisho, ubanaji hufanyika kwa sababu za kimaadili na kitaadhima.



Marejeleo

- Annah, N. K. (2023). *Upanuzi na Ubanaji wa Maana katika Kandanda: Ulinganisho na Ulinganuzi Nchini Kenya na Tanzania* (Masters Dissertation, University of Nairobi).
- Asiko, A. F. (2019). *Ushawishi wa Kiasi cha Habari Kinachopitishwa katika Tafsiri* (Masters Dissertation, University of Nairobi).
- Blutner, R. (1998). Lexical Pragmatics. *Journal of Semantics*, 15(2), 115-162.
- Blutner, R. (2000). Some Aspects of Optimality in Natural Language Interpretation. *Journal of Semantics*, 17(3), 189-216.
- Horn, L. (2005). Current Issues in Neo-Gricean Pragmatics. *Intercultural Pragmatics*, 2:191-204.
- Katui, S. P. (2020). *Uchanganuzi wa Kipragmatiki wa Maana ya Mawasiliano katika Jukwaa la Facebook* (Masters Dissertation, University of Nairobi).
- Kirui, S. K. (2021). *Urejelezi katika Gazeti la Taifa Leo: Mtazamo wa Kipragmatiki* (Masters Dissertation, University of Nairobi).
- Kiunga, T. M. (2016). *Maana ya Usemi na Mazungumzo katika Mitandao ya Kijamii, Hususan Facebook na Twitter* (Masters Dissertation, University of Nairobi).
- Mkude, D. J. (1995). *Towards a Semantic Typology of Swahili Language*. (Unpublished M.A Thesis of University of Nairobi).
- Mmbawanga, K.F (2010). *New Words and Meaning on Facebook: A Lexical Pragmatics Analysis*. (Masters Dissertation, University of Nairobi).
- Nkumbo, D., Wandera-Simwa, S., & Ogola, J. O. (2019). Uchambuzi wa Maudhui katika Matangazo ya Ngoni-salama kwenye Ukurasa wa Shabiki wa Durex Facebook. *Editon Consortium Journal of Kiswahili*, 1(1), 29-37.
- Ochoki, B. M. (2010). *Pragmatic Interpretation Constraints in Kenyan Hip Hop Lyrics* (Doctoral Dissertation, University of Nairobi).
- TUKI. (1990). *Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha*. Educational Publishers and Distributors.
- Wilson, D. & Carson, R. (2007). *A Unitary Approach to Lexical Pragmatics: Relevance Influence and ad hoc Concepts*.
- Wilson, D. (2003). Relevance and Lexical Pragmatics. *Italian Journal of Linguistics*, 15, 273-292.